



MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR

**S.L.P. 3650
VICTORIA GARDEN
ZANZIBAR**

**SIMU: 024 223 2916
MOB: 0774 824242
FAX: 024 223 1461**

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), imesema maendeleo ya Zanzibar yanaweza kufikiwa kwa kiasi kikubwa endapo kutakuwa na udhibiti mpana wa kutokomeza vitendo vya rushwa kupitia Nyanja mbalimbali za kimaendeleo.

Mkurugenzi wa Idara ya **Kinga dhidi ya Rushwa** kutoka ZAECA Makame Khamis Hassan alisema hayo Ofisini kwake Victoria Garden Vuga alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kutoka vyombo mbalimbali kufuatia maadhimisho ya **siku ya mapambano dhidi ya rushwa Afrika** ambayo hufanyika kila mwaka ifikapo **Julai 11**.

Alisema kuendelea kushamiri kwa vitendo hivyo kupitia maeneo mbalimbali ndio kunakosababisha kuviza shughuli za maendeleo ndani ya visiwa hivi na kuwafanya wananchi wake kuendelea kuwa maskini kutokana na kukosekana kwa huduma nyingi za kimaendeleo.

Sambamba na hayo alifahamisha kwamba kuanzia kipindi cha Julai 2020 hadi Juni 2021 Mamlaka hiyo ilipokea malalamiko 382, kati ya hayo 280 ni tuhuma ambazo

zinaendelea kufanyiwa uchunguzi, kati ya hizo tuhuma 59 zimefungwa baada ya kukosekana ushahidi.

Aidha alifahamisha kwamba majalada 29 yameshafikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa hatua zaidi za kisheria na majalada 18 yamehamishiwa taasisi zinazohusiana na tuhuma hizo.

Mkurugenzi huyo alizidi kufafanua kwamba tuhuma 15 zimefanyiwa udhibiti kutokana na kutokamilika ushahidi ili kuweza kutoa njia sahihi za kiutendaji katika sekta husika, huku tuhuma 33 zimetolewa ushauri na tuhuma 5 zimewasilishwa mahakamani na kesi 4 zimetolewa maamuzi.

“Miongoni mwa tuhuma hizo kuna zile zinazohusisha miradi mbali mbali ikiwemo ZUSP, tuhuma zinazohusu vikosi vya SMZ kama vile JKU na Kikosi cha Zima Moto na Uokozi, Kesi zinazohusu Wizara ya Fedha, Jumba la Treni, ZECO, MASTERLIFE, Manunuzi hewa ya mbolea ya KOREA,” alisema.

Aidha alifahamisha kwamba katika maeneo hayo kunatuhuma tofauti ikiwemo kufanya ubadhirifu wa mali na mapato, matumizi mabaya ya ofisi, kutokufuata taratibu za manunuzi, kukwepa kulipa kodi ambapo uchunguzi wa majalada ya kesi hizi unaendelea.

Mbali na hayo Mkurugenzi huyo alisema kwa kipindi hicho Mamlaka hiyo imefanikiwa kuokoa jumla ya shilingi milioni 411,348,724.30/= za Kitanzania ambazo zilikuwa zitumike kinyume na utaratibu.

“Baada ya kufanya uchunguzi tumegundua kwamba fedha hizo zilihusisha tuhuma mbalimbali ikiwemo kukwepa kulipa kodi, ubadhirifu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali,” alisema.

Alifahamisha kwamba Serikali itaendelea kukabiliana ipasavyo na vitendo vya rushwa, ufisadi na ubadhirifu wa mali za umma kwa kuwachukulia hatua watakao thibitika kufanya vitendo hivyo ili kuifanya nchi iweze kuendelea.

Akitaja baadhi ya maeneo ambayo yamekuwa yakikabiliwa kwa kiasi kikubwa na vitendo hivyo Mkurugenzi huyo alisema katika maeneo ya huduma za kijamii kumeenea kwa kiasi kikubwa vitendo hivyo, hali ambayo inawafanya wananchi wanyonge kushindwa kuzipata huduma hizo kwa ufanisi.

Akizungumzia mikakati yao alisema wataendelea kuwajengea uwezo watumishi wao ili kuwa na uwezo mkubwa wa kupambanua na kudhibiti vitendo hivyo kwa maslahi ya taifa.

Hata hivyo alitumia fursa hiyo kuwataka wananchi, taasisi na wadau mbalimbali kuunga mkono jitihada na mapambano dhidi ya vitendo hivyo kupitia ngazi tofauti ili kuhakikisha rushwa inapungua na hatimae kumalizika kabisa.

Siku ya mapambano dhidi ya rushwa Afrika hufanyika kila mwaka ifikapo Julai 11, ambapo kaulimbiu ya mwaka huu ni “Jumuia za kiuchumi za kikanda ni wadau muhimu katika utekelezaji wa mkataba wa kuzuia na kupambana na rushwa wa umoja wa afrika”.